

## **TANGAZO KWA UMMA**

### **MIKOPO YA PEMBEJEZO ZA UFUGAJI SAMAKI KWA VIZIMBA AWAMU YA PILI**

Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) inakaribisha maombi ya mkopo wa masharti nafuu. Mkopo huo unalenga kutoa pembejezo za ufugaji samaki kwa vizimba kibiashara katika Ziwa Victoria. Mkopo utajumuisha vizimba vya mviringo vya plastiki na chuma vyenye kipenyo cha mita 6, 8 na 10; vifaranga vya sato; na chakula cha samaki. Walengwa ni vyama vya ushirika/vikundi, makampuni na watu binafsi wanaokidhi vigezo.

Maombi yaambatanishwe na andiko la biashara pamoja na muhtasari wa kikao ulioridhia kukopa na ukomo wa madeni kwa vyama vya ushirika; barua ya dhamana kutoka halmashauri husika kwa vikundi; na dhamana ya mkopo kwa mtu binafsi na kampuni. Maelezo ya kina yanapatikana katika tovuti ya Wizara [www.mifugouvuvি.go.tz](http://www.mifugouvuvি.go.tz), Ofisi za Uvuvi katika Halmashauri husika na Ofisi za Wizara zinazoshughulika na masuala ya Uvuvi.

Maombi yote yaidhinishwe na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri husika na kutumwa kwa Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi **kabla ya tarehe 29 Januari, 2024** kuitia anuani ifuatayo;

KATIBU MKUU  
WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI  
S.L.P 2847  
40487-DODOMA  
Simu: +255 26 23 22613  
Baruapepe: [ps@uvuvi.go.tz](mailto:ps@uvuvi.go.tz)